

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

ANUANI YA SIMU:
"UHAMIAJI"

TELEFAX:+255 22 2850595

+255 22 2850584



OFISI YA KAMISHINA
JENERALI WA UHAMIAJI,

S . L . P. 512,

Dar-es-salaam.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Nchini Dr. Anna Peter Makakala amefanya mabadiliko makubwa ya Viongozi wa Uhamiaji wa Mikoa mbalimbali hapa nchini pamoja na kuwateua Wakuu Wapya wa mikoa kushika nyadhifa hizo katika Mikoa iliyopo Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

Katika Mabadiliko haya Naibu Kamishna wa Uhamiaji Sixstus Faustine Nyaki aliyekuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza amehamishiwa mkoa wa Simiyu wakati aliyekuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Rukwa Naibu Kamishna wa Uhamiaji Selemani Bandiho Kameya amehamishiwa Mkoa wa Tabora.

Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Asumsio Paulus Achacha amehamishiwa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Manyara Naibu Kamishna Peter Jerome Kundy amehamishiwa Mkoa wa Dodoma kuchukua nafasi ya Kamishna Msaidizi Ali Mohamed ambaye amehamishiwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji mkoa wa Arusha.

Naibu Kamishna wa Uhamiaji Mkemi Mhina Seif ameteuliwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Kusini Unguja, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Muhsin Abdallah Muhsin ameteuliwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Kaskazini Unguja, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Said Omary Hamdani ameteuliwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi na Naibu Kamishna wa Uhamiaji Othman Khamis Salum ameteuliwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mjini Magharibi Unguja.

Katika mabadiliko hayo baadhi ya Wakuu wa Uhamiaji wa Mikoa wamebaki katika Vituo vyao vya kazi vya awali akiwemo aliyekuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Morogoro

Naibu Kamishna wa Uhamiaji Safina Muhindi, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Lindi Naibu Kamishna wa Uhamiaji George Kombe, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Ruvuma Naibu Kamishna wa Uhamiaji Hilgaty Laurent Shauri, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Singida Naibu Kamishna wa Uhamiaji Faith Alexander Ihano na Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mara Naibu Kamishna Fredrick Eustace Kiondo.

Wengine waliobaki kwenye vituo vyao vya awali ni pamoja na Naibu Kamishna wa Uhamiaji Abdallah Ramadhani Towo mkoa wa Kagera na Naibu Kamishna wa Uhamiaji Anastazia Gasper Ngatunga mkoa wa Shinyanga.

Katika mabadiliko hayo Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dr. Makakala pia amewateua Viongozi wa Uhamiaji wa Mikoa wapya katika baadhi ya mikoa hapa nchini ambapo Naibu Kamishna wa Uhamiaji Mary Francis Palmer kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Placid Mazengo, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Pwani, Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji James Andrew Mwanjotile, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Hope Jaffer Kawawa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Iringa, na Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji Hosea Alphonse Kagimbo Mkoa wa Njombe.

Wengine ni Naibu Kamishna wa Uhamiaji Rashid Salum Magetta Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Songwe, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Carlos John Haule, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Rukwa, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Julieth Deodatus Sagamiko Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Manyara, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Albert Joseph Rwelamila, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Kilimanjaro na Naibu Kamishna wa Uhamiaji Paul Laurent Eranga, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza.

Naibu Kamishna wa Uhamiaji Crispin Crispin Ngonyani ameteuliwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Tanga, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Shaban Omar Hatibu Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Katavi, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Remigius Ibrahimu Pesambili Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Kigoma na Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji Novaita Edmund Mrosso ameteuliwa kuwa Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Mbeya.

Aidha Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji Bakari Mohamed Ameir ameteuliwa kuwa Mkuu wa Kituo cha Uhamiaji cha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume [AAKIA] na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhamiaji Fulgence Andrew Mutarasha kuwa Mkuu wa Uhamiaji Kituo cha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere[JNIA].

Imetolewa na
Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Nchini
Dr. A. P. Makakala
3 Machi 2017